# NATAMANI

*Jerome Mwaya*






**2.Sogea karibu Yesu, niseme nawe, (Niseme nawe), Nisimulie kidogo mambo ya mbinguni. Tusemezane habari, za mji ule (za mji ule), uliojengwa mbinguni na Mungu mwenyewe.**

**3.Ninatamani kuona, mji wa Mungu, (mji wa Mungu) Uliopambwa kwa nuru ya Mwanakondoo. Ninatamani kuona, na jina langu (na jina langu), Limo katika kitabu cha watakatifu.**

**4.Ninatamani kumwona, Mama Maria (Mama Maria), Niambatane na Petro na Mitume wote. Nionesheni Eliya, na Manabii (na Manabii), Nitembezeni mbinguni enyi Malaika.**